

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 65 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** JULAI 2026

TSC YATUNUKIWA TUZO KWA MCHANGO WAKE KATIKA KUIMARISHA UTUMISHI WA UMMA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (kulia), akimkabidhi Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tuzo ya kutambua mchango wa Tume katika kuimarisha Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora, wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

TUZO YA TSC IENDELEE KUWA CHACHU YA KUONGEZA BIDII NA UBORA WA HUDUMA

Hongera kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kutunukiwa tuzo maalum inayotambua mchango wake katika kuimarisha Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora nchini. Tuzo hii ni heshima kwa taasisi na uthibitisho kwamba juhudi zinazowekwa kila siku katika kuwahudumia walimu na kusimamia masuala yao ya kiutumishi zinaonekana na kuthaminiwa katika ngazi ya kitaifa.

Pongezi za dhati ziendee uongozi wa Tume ukiongozwa na Mwenyekiti, Prof. Masoud Hadi Muruke na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, pamoja na watumishi wote wa TSC kwa ushirikiano, weledi na kujituma kwao. Mafanikio haya si ya mtu mmoja bali ni matokeo ya mshikamano, uwajibikaji na dhamira ya pamoja ya kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi matarajio ya walimu na wananchi kwa ujumla.


Aidha, tuzo hii iwe chachu ya kuongeza ari ya ubunifu, matumizi ya teknolojia na kuendelea kujenga utamaduni wa uwazi na uwajibikaji katika

utekelezaji wa majukumu ya Tume. Mafanikio ya leo yanapaswa kuwa msingi wa kutafuta mafanikio makubwa zaidi, hususan katika kipindi ambacho Taifa linaelekea kutekeleza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Hata hivyo, mafanikio haya yanaambatana na wajibu mkubwa zaidi. Watumishi wa Tume wanapaswa kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, weledi na kujituma, wakitambua kuwa matarajio ya walimu na wadau yataendelea kuongezeka kadiri Tume inavyozidi kujijengea imani mbele ya umma. Kila mmoja aendelee kuwa balozi wa huduma bora na mfano wa maadili mema katika Utumishi wa Umma.

Tunawatakia uongozi na watumishi wote wa TSC kila la heri katika kuendeleza mafanikio haya. Tuendeleo kushirikiana, kuthaminiana na kutekeleza majukumu yetu kwa moyo wa uzalendo na uwajibikaji ili Tume iendeleo kuwa taasisi ya mfano katika utoaji wa huduma bora na mchango wake katika maendeleo ya sekta ya elimu na Taifa kwa ujumla.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Apsa Othman
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

TSC YATUNUKIWA TUZO KWA MCHANGO WAKE KATIKA KUIMARISHA UTUMISHI WA UMMA

**Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetunukiwa tuzo maalum kwa kutambua mchango wake katika kuimarisha Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora nchini.

Tuzo hiyo ilitolewa tarehe 18, 2026, wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, likiwa na dhima isemayo "Nafasi ya Utumishi wa Umma katika Kufanikisha Malengo ya Dira za Taifa 2050."

Kongamano hilo lililoandaliwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar (ZIPA), lililenga kujadili namna bora ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Utumishi wa Umma ili kuchangia kufikiwa kwa malengo ya Dira za Taifa 2050 (kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar).

Mgeni rasmi katika kongamano hilo alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, aliyemwakilisha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, alihudhuria kongamano hilo na kupokea tuzo hiyo kwa niaba ya Tume kutoka kwa Mhe. Kikwete.

Akizungumza mara baada ya kupokea tuzo hiyo, Mwl. Nkwama alisema Tume inapokea tuzo hiyo kwa unyenyekevu mkubwa na kuiona kama ishara ya kuthamini jitihada zinazofanywa katika kuimarisha Utumishi wa Umma na utoaji wa huduma bora kwa walimu nchini.

"Tuzo hii ni chachu na motisha kwetu kuendelea kuboresha huduma tunazozitoa kwa walimu na wadau wetu kwa weledi, ufanisi na uwajibikaji zaidi," alisema Mwl. Nkwama.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (kulia), akimkabidhi Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tuzo ya kutambua mchango wa Tume katika kuimarisha Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora, wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambapo washiriki walijadili nafasi ya Utumishi wa Umma katika kufanikisha utekelezaji wa Dira za Taifa 2050.

Katika kongamano hilo mada mbili ziliwasilishwa na kujadiliwa ambapo mada ya kwanza ilikuwa ni "Nafasi ya Utumishi wa Umma katika Kukuza Ubora wa Taasisi Nchini na Kuchangia Utekelezaji wa Dira za Taifa 2050 kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar," iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum.

Mada nyingine ilikuwa "Mchango wa Ubunifu na Mabadiliko ya Kidijitali ndani ya Utumishi wa Umma katika Kuchochea Utekelezaji wa Dira za Taifa 2050," iliyowasilishwa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mhe. Prof. Kitila Mkumbo.

Akizungumza katika kongamano hilo, Mhe. Ridhiwani Kikwete alisema Utumishi wa Umma unaotarajiwa ni ule unaoshirikiana na wadau mbalimbali katika kuhudumia wananchi, huku akisisitiza umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika mafunzo kwa watumishi wa

umma na kuimarisha matumizi ya tafti katika kufanya maamuzi na kuboresha utendaji.

Alieleza kuwa matumizi ya tafti, ubunifu na mabadiliko ya kidijitali ni nyenzo muhimu zitakazosaidia kuongeza tija na kuhakikisha Utumishi wa Umma unaendelea kuwa mhimili muhimu wa maendeleo ya Taifa kuelekea mwaka 2050.

Naye Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Prof. Masoud Hadi Muruke, alizitaka taasisi za umma kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ubunifu na bidii huku zikizingatia utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Prof. Muruke alisema kuwa mafanikio ya Dira ya Taifa 2050 hayawezi kupatikana bila kuwa na Utumishi wa Umma imara unaotanguliza maslahi ya wananchi na maendeleo ya Taifa.

Kutunukiwa kwa TSC tuzo hiyo kunathibitisha mchango wa Tume katika kuimarisha Utumishi wa Umma na ni motisha ya kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi, uwajibikaji na ufanisi ili kuhakikisha walimu nchini wanapata huduma bora zinazochangia maendeleo ya sekta ya elimu na Taifa kwa ujumla.

TSC YATUNUKIWA TUZO KWA MCHANGO WAKE KATIKA KUIMARISHA UTUMISHI WA UMMA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhizwani Jakaya Kikwete (kulia), akimkabidhi Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tuzo ya kutambua mchango wa Tume katika kuimarisha Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora, wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akionesha tuzo iliyotolewa kwa Tume kwa kutambua mchango wake katika kuimarisha Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora, wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhizwani Jakaya Kikwete akitoa hotuba ya ufunguzi wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.

TSC YATUNUKIWA TUZO KWA MCHANGO WAKE KATIKA KUIMARISHA UTUMISHI WA UMMA



Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa salamu wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali walioshiriki Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.

TSC YATUNUKIWA TUZO KWA MCHANGO WAKE KATIKA KUIMARISHA UTUMISHI WA UMMA



Baadhi ya washiriki wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania wakifuatilia mada mbalimbali zilizowasilishwa katika kongamano hilo lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (wa nne kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto), pamoja na Kaimu Makatibu Wasaidizi wa Tume kutoka wilaya mbalimbali za Mkoa wa Dar es Salaam, wakiwa katika picha ya pamoja wakionesha tuzo iliyotumukiwa Tume wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania, lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (wa nne kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto), pamoja na Kaimu Makatibu Wasaidizi wa Tume kutoka wilaya mbalimbali za Mkoa wa Dar es Salaam, wakifurahia tuzo iliyotumukiwa Tume wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania, lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (wa nne kutoka kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto), pamoja na Kaimu Makatibu Wasaidizi wa Tume kutoka wilaya mbalimbali za Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania, lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Kaimu Makatibu Wasaidizi wa Tume kutoka wilaya mbalimbali za Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa Kongamano la Pili la Utumishi wa Umma Tanzania, lililofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar es Salaam, Juni 18, 2026.

TSC YASHIRIKI WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, YATOA HUDUMA KWA WANANCHI DODOMA

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni miongoni mwa taasisi za Serikali zinazoshiriki Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi kupitia mabanda yaliyowekwa katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

Maadhimisho hayo ya utoaji huduma kwa wananchi yanafanyika kuanzia Juni 16 hadi 23, 2026 chini ya kaulimbiu isemayo "Kuchochea Uwajibikaji Jumuishi kwa Huduma Endelevu."

Maadhimisho hayo yalifunguliwa rasmi tarehe 17 Juni, 2026 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete.

Akizungumza wakati wa ufunguzi huo, Mhe. Kikwete aliwapongeza watumishi wa umma kwa kuendelea kutoa huduma kwa wananchi kwa kujituma na weledi, huku akiwataka kutumia fursa wanazopata kuwaelimisha wananchi kuhusu mafanikio na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuwaletea maendeleo.

Alisema ni muhimu wananchi wakafahamu namna Serikali yao inavyowajibika na mchango wa taasisi mbalimbali katika kuboresha huduma na kuinua ustawi wa wananchi.

Hafu ya ufunguzi ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, akiwemo Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, ambaye aliongoza ushiriki wa Tume katika maadhimisho hayo yanayolenga kuimarisha uwajibikaji na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Katika kipindi chote cha maadhimisho, Tume ya Utumishi wa Walimu inaendelea kutoa huduma na elimu kwa walimu na wananchi kuhusu majukumu yake, taratibu mbalimbali za utumishi wa walimu pamoja na kushughulikia changamoto na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya elimu.

Ushiriki wa TSC katika Wiki ya Utumishi wa Umma unaakisi dhamira ya Serikali ya kuimarisha utoaji wa huduma bora, kuongeza uwazi na kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi kupitia taasisi zake.

Wananchi, walimu na wadau



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akisaini daftari la wageni alipotembelea banda la Tume katika maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, tarehe 17 Juni, 2026, kwenye viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Nuhu Mlekwa (kulia), akitoa huduma kwa mteja aliyetembelea banda la Tume wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

mbalimbali wamekaribishwa kutembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu lililopo katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma ili kupata huduma na kujifunza zaidi kuhusu shughuli na majukumu ya Tume.

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma hutoa fursa kwa taasisi za umma kuonesha huduma wanazozitoa na mchango wake katika maendeleo ya taifa, sambamba na kuimarisha uhusiano kati ya Serikali na wananchi.

TSC YASHIRIKI WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, YATOA HUDUMA KWA WANANCHI DODOMA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati, waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa Tume kwenye banda la TSC wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, tarehe 17 Juni, 2026, katika vizwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Sylver Igogo (kushoto), akitoa huduma kwa mteja aliyetembelea banda la Tume wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika vizwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.



Baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika banda la Tume wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika vizwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

TSC YASHIRIKI WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, YATOA HUDUMA KWA WANANCHI DODOMA



Baadhi ya washiriki, wakiwemo watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakifuatilia hafla ya ufunguzi wa Wiki ya Utumishi wa Umma iliyofanyika tarehe 17 Juni, 2026, katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

KATIBU WA TSC ASISITIZA UMUHIMU WA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, amesema Wiki ya Utumishi wa Umma ni fursa muhimu inayoweza taasisi za Serikali kusogeza huduma karibu na wananchi na kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili ili kuzitafutia ufumbuzi kwa wakati.

Mwl. Nkwama aliyasema hayo Juni 16, 2026, alipotembelea na kutoa huduma kwa mteja katika banda la Tume lililopo katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma, ambako maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanaendelea yakiwa na kaulimbiu isemayo, "Kuchochea Uwajibikaji Jumuishi kwa Huduma Endelevu."

Alisema maadhimisho hayo yanatoa nafasi kwa wananchi, wakiwemo walimu na wadau wa elimu, kupata huduma mbalimbali na ufafanuzi wa masuala yanayohusu utumishi wa walimu bila kulazimika kufika katika ofisi za Tume.

"Wiki ya Utumishi wa Umma ni jukwaa muhimu linalowakutanisha watoa huduma na wananchi, hivyo linatoa fursa ya kusikiliza maoni, kupokea changamoto na kutoa ufumbuzi wa masuala mbalimbali kwa haraka zaidi," alisema Mwl. Nkwama.

Aliongeza kuwa Tume itaendelea kutumia maadhimisho hayo kuelimisha umma kuhusu majukumu yake na kuhakikisha huduma zinazotolewa zinawafikia walimu na wananchi kwa ufanisi na kwa kuzingatia misingi ya uwajibikaji.

Tume ya Utumishi wa Walimu ni miongoni mwa taasisi za Serikali zinazoshiriki maadhimisho hayo yanayofanyika kuanzia Juni 16 hadi 23, 2026 katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma, ambapo wananchi wanapata fursa ya kupata huduma na elimu kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi za umma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akitoa huduma kwa mteja aliyetembelea banda la Tume kwenye maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Mteja tarehe 16 Juni, 2026 jijini Dodoma.

MBOZI WAIPONGEZA TSC KWA MAFANIKIO YA MIAKA 10 YA UTOAJI HUDUMA

Na Mwandishi Wetu, Mbozi

Baadhi ya walimu wa Wilaya ya Mbozi wameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016, wakisema imeimarisha utoaji wa huduma na kuboresha ustawi pamoja na mazingira ya kazi kwa walimu nchini.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Haloli, iliyoipo Kata ya Vyawa, Mwl. Subira Abasi Mngano, alisema kabla ya kuanzishwa kwa TSC, walimu walikumbwa na changamoto nyingi za kiutumishi ambazo zilichukua muda mrefu kushughulikiwa.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Haloli, Mwl. Subira Abasi Mngano, akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu.

Kwa upande wake, Mwalimu Judith alisema kuanzishwa kwa TSC kumeongeza ari na morali ya kazi kwa

walimu kutokana na kuboreshwa kwa utoaji wa huduma mbalimbali za kiutumishi.

Alieleza kuwa katika kipindi cha miaka 10 ya TSC, walimu wengi wamekuwa wakipandishwa vyeo na kubadilishiwa miundo kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa awali walipokuwa wakihudumiwa chini ya Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD).

“Moja ya mambo yaliyoongeza ari ya walimu ni kulipwa kwa wakati stahili zao za kisheria, ikiwemo nauli za likizo, posho za kujikimu kwa walimu wa ajira mpya, stahili za uhamisho pamoja na malimbikizo ya mishahara baada ya kupanda vyeo. Hali hii imeleta faraja na kuongeza motisha wa kufanya kazi,” alisema.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Ndugu, Mwl. Cosmas Wilson Nzoa, alisema TSC imewasaidia walimu kuelewa vizuri haki, wajibu na maadili ya utumishi kupitia miongozo mbalimbali inayotolewa na kusambazwa mara kwa mara.

Alisema miongozo hiyo imerahisisha utendaji kazi shuleni na kuchangia kupungua kwa mashauri ya nidhamu miongoni mwa walimu.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Ndugu, Mwl. Cosmas Wilson Nzoa, akizungumza kuhusu mafanikio ya miaka 10 ya TSC.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Sekondari Ivwanga, Mwl. David Bubinza Simba, aliishukuru TSC kwa kusimamia kwa ufanisi mabadiliko ya miundo kwa walimu wanaojiendeleza kielimu, jambo ambalo limeongeza motisha na kuwapa moyo wa kuendelea kujiendeleza kitaaluma.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Ivwanga, Mwl. David Bubinza Simba, akielezea namna TSC ilivyoboreshwa huduma za kiutumishi kwa walimu.

MBOZI WAIPONGEZA TSC KWA MAFANIKIO YA MIAKA 10 YA UTOAJI HUDUMA

Akizungumzia mafanikio ya taasisi, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mbozi, Bw. Pendo Lutangilo Mnyalape, alisema katika kipindi cha miaka 10 Tume imeziwezesha ofisi za wilaya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kupitia uboreshaji wa mazingira ya kazi.

Alisema TSC imeweza upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA, ikiwemo kompyuta za mezani, kompyuta mpakato (laptop), printa na huduma za mawasiliano ya mtandao zinazoweza matumizi

ya mifumo mbalimbali ya kidijitali ikiwemo TSCMIS na PEPMIS.

Aidha, alisema Tume imeendelea kutoa fedha za uendeshaji wa ofisi, kugharamia vikao vya kisheria, vifurushi vya mawasiliano pamoja na mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya, hatua ambayo imeongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Bw. Mnyalape aliongeza kuwa katika kipindi hicho pia kumekuwa na ushirikiano mzuri kati ya TSC na taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi wa elimu, ikiwemo wakuu wa shule, Ofisi za Wathibiti

Ubora wa Shule pamoja na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri, Miji, Manispaa na Majiji, hali iliyorahisisha utekelezaji wa majukumu ya kiutumishi kwa walimu.

Naye Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Wilaya ya Mbozi, Bi. Judith Musyani, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa Tume kupitia maboresho ya miundo ya utumishi, hatua ambayo amesema imeongeza morali, uwajibikaji na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mbozi, Bw. Pendo Lutangilo Mnyalape, akizungumza wakati wa mahojiano maalumu na Afisa kutoka TSC Makao Makuu.



Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Wilaya ya Mbozi, Bi. Judith Musyani.



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mbozi wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu.

MIAKA 10 YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YALETA MABADILIKO CHANYA KWA WALIMU WILAYANI ILEJE

Na Mwandishi Wetu, Ileje

Walimu wa Wilaya ya Ileje mkoani Songwe wameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, wakisema huduma zinazotolewa zimeboresha ustawi wao na kurahisisha utatuzi wa changamoto mbalimbali za kiutumishi.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Nyerere iliyopo Kata ya Itumba, Bi. Rehema Mwambene Lwinda, alisema Tume imeleta mageuzi makubwa katika usimamizi wa masuala ya kiutumishi, hususan upandishaji wa madaraja.

Alieleza kuwa kabla ya kuanzishwa kwa Tume, walimu walikuwa wakikaa kwa muda mrefu katika daraja moja bila kupandishwa. Akitoa mfano wa uzoefu wake binafsi, alisema alijiririwa mwaka 1990 lakini alipandishwa daraja la kwanza mwaka 1996, baada ya kusubiri kwa miaka sita.

"Enzi hizo tulilazimika kuandika barua za kukubali kupandishwa daraja na kuzisafirisha umbali mrefu hadi mamlaka husika, kisha kusubiri majibu kwa muda mrefu. Kwa sasa huduma zimesogezwa karibu na walimu, hivyo upandishaji wa madaraja unafanyika kwa wakati na bila usumbufu mkubwa," alisema.

Bi. Lwinda pia aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuhakikisha walimu wanalipwa mishahara na stahiki nyingine kwa wakati, jambo ambalo amesema limeongeza ari na morali ya kufanya kazi.

Naye Mwalimu wa Shule ya Sekondari Itumba, Bw. Didiye John Paul, alisema kuanzishwa kwa Tume kama chombo chenye mamlaka ya kufanya maamuzi kuhusu masuala ya kiutumishi kumeongeza uwazi, haki na ufanisi katika kushughulikia changamoto za walimu.

Alisema utaratibu wa upandishaji vyeo na kushughulikia masuala mengine ya kiutumishi kwa wakati umeongeza hamasa kwa walimu kufanya kazi kwa bidii na kujituma zaidi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Wilaya

ya Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu, Mwl. Alfacksaid Stafford Kibona, alisema katika kipindi cha miaka 10 ya Tume kumekuwa na mafanikio makubwa katika usimamizi wa rasilimali watu kwa kada ya ualimu.

Alieleza kuwa moja ya mafanikio hayo ni kuimarika kwa mfumo wa Kamati za Wilaya zenye mamlaka ya kufanya maamuzi kuhusu ajira, upandishaji vyeo na mashauri ya kinidhamu, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo maamuzi mengi yalifanywa na ngazi za juu.

Aidha, aliipongeza Tume kwa kuendelea kutoa mafunzo elekezi kwa wajumbe wa kamati hizo, jambo ambalo limewaongezea uelewa wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu.

"Mafunzo haya yameongeza uwezo wa kamati kuendesha mashauri ya walimu kwa weledi na kupunguza dosari zilizokuwa zikisababisha baadhi ya mashauri kuanza upya kutokana na kutokuzingatia taratibu," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ileje, Mwl. Deogratius Lucas Mhume, alisema katika kipindi cha miaka 10 ya Tume kumekuwa na maboresho makubwa katika utoaji wa huduma kwa walimu kupitia matumizi ya teknolojia.

Alisema matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) yamerahisisha utekelezaji wa majukumu katika ofisi za TSC ngazi ya wilaya, ikiwemo usajili wa walimu, utoaji wa namba za TSC, maandalizi ya barua za ajira pamoja na mikataba ya kazi.

"Mfumo huu umeongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu kwa kupunguza muda wa kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutumishi," alisema.

Aliongeza kuwa Tume itaendelea kuboresha huduma zake kwa kutumia teknolojia na kuimarisha mfumo ya kiutendaji ili kuhakikisha walimu wanapata huduma bora, za haraka na zenye kuzingatia misingi ya haki na uwazi.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ileje, Bw. Deogratius Lucas Mhume, akiwa ofisini kwake wakati wa mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu.



Mwenyekiti wa Kamati ya Wilaya ya Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ileje, Mwl. Alfacksaid Stafford Kibona.

MIAKA 10 YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YALETA MABADILIKO CHANYA KWA WALIMU WILAYANI ILEJE



Mwalimu wa Shule ya Msingi Nyerere, Bi. Rehema Mwambene Lwanga, akizungumza na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (hayupo pichani) kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu alipotembelea shuleni hapo.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Itumba, Bw. Didiye John Paul, akizungumza na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (hayupo pichani) kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu.

MWL. NKWAMA AWAHIMIZA WATUMISHI WA TSC KUDUMISHA USHIRIKIANO NA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu, Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, amewahimiza watumishi wa Tume Makao Makuu kuendelea kuimarisha ushirikiano, kuongeza uelewa wa pamoja kuhusu majukumu ya Tume na kushiriki kikamilifu katika kuboresha utendaji kazi ili kuhakikisha huduma bora zaidi zinatolewa kwa walimu nchini.

Mwl. Nkwama alitoa rai hiyo Juni 24, 2026, wakati akifungua kikao Kazi cha watumishi wa Tume Makao Makuu kilichofanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC), jijini Dodoma.

Alisema lengo la kikao kazi hicho ni kutoa fursa kwa watumishi kushirikishana taarifa, mafanikio, changamoto na fursa mbalimbali ili kuendelea kuboresha utendaji kazi na kuhakikisha Tume inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

"Kila mtumishi anapaswa kuwa na uelewa kuhusu majukumu ya msingi ya Tume. Tunapofahamu tunachokifanya na kila mmoja akielewa nafasi yake, tutatoa huduma bora zaidi na kuzungumza lugha moja katika kuwahudumia walimu na wadau wetu," alisema Mwl. Nkwama.

Aliwapongeza watumishi kwa juhudi na kujituma kwao katika kutekeleza majukumu yao, akibainisha kuwa mchango wao umeiwezesha Tume kupata tuzo ya kutambua mchango wake katika kuimarisha Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora.

Aidha, alisisitiza kuwa kikao kazi hicho ni cha ushirikishwaji, hivyo kila mtumishi ana wajibu wa kushiriki kikamilifu kwa kutoa maoni, mapendekezo na uzoefu wake kwa lengo la kuendelea kuimarisha utendaji wa



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua kikao kazi na Watumishi wa Tume Makao Makuu kilichofanyika tarehe 24 Juni, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC), jijini Dodoma.

Tume.

Katika kikao kazi hicho, Wakuu wa Idara na Vitengo waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika maeneo wanayosimamia, hatua iliyotoa fursa kwa watumishi kupata uelewa mpana kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Tume na namna zinavyochangia kufikiwa kwa malengo ya taasisi.

Kikao kazi hicho ni sehemu ya jitihada za Tume ya Utumishi wa Walimu za kuendelea kujenga utamaduni wa uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji miongoni mwa watumishi wake kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa walimu na wadau wengine wa sekta ya elimu.



Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia masuala ya Utawala Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Apsa Othman akitoa neno la utangulizi wakati wa kikao kazi cha Katibu wa Tume na Watumishi wa Tume Makao Makuu kilichofanyika tarehe 24 Juni, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC), jijini Dodoma.

MWL. NKWAMA AWAHIMIZA WATUMISHI WA TSC KUDUMISHA USHIRIKIANO NA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU



Baadhi ya watumishi wa Tume wakiwa katika kikao kazi na Katibu wa Tume kilichofanyika tarehe 24 Juni, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC), jijini Dodoma.

MWL. NKWAMA AWAHIMIZA WATUMISHI WA TSC KUDUMISHA USHIRIKIANO NA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU



Baadhi ya watumishi wa Tume wakiwa katika kikao kazi na Katibu wa Tume kilichofanyika tarehe 24 Juni, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC), jijini Dodoma.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YATOA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WA AJIRA MPYA WILAYANI KISARAWA

Na Mwandishi Wetu, Kisarawe

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kisarawe imetoa mafunzo elekezi kwa walimu 95 wa ajira mpya kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao, hatua iliyochangia kuongeza uelewa wa walimu hao kuhusu haki, wajibu na maadili ya utumishi wa umma.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kisarawe, Bi. Sophia Hussein Kizenga, wakati wa mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali katika kipindi cha miaka kumi ya TSC.

Bi. Sophia alisema kati ya walimu hao, 30 ni wa shule za msingi na 65 ni wa shule za sekondari. Alieleza kuwa mafunzo hayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza makosa ya kinidhamu na kuwajengea walimu uelewa wa majukumu yao katika utumishi wa umma.

"Mafunzo elekezi ni miongoni mwa mafanikio makubwa ya kujivunia katika kipindi cha miaka kumi ya uwepo wa TSC. Yameleta tija kubwa katika utumishi wa walimu, jambo ambalo halikuwepo hapo awali. Zamani mwalimu alikuwa akipangiwa kituo cha kazi na kuanza majukumu bila kupewa maelekezo kuhusu wajibu, haki na stahili zake kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi," alisema.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa mafunzo hayo umechangia kupungua kwa mashauri ya nidhamu wilayani humo, ambapo mwaka wa fedha 2015/2016 kulikuwa na mashauri 42, huku kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yakishuka hadi wastani wa mashauri mawili pekee.

Aidha, alisema Serikali imeendelea kuiwezesha TSC kwa kuipatia rasilimali fedha kwa ajili ya kuendesha



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kisarawe wakiwa katika picha ya pamoja nje ya ofisi za TSC Kisarawe. Kutoka kulia ni Bw. Michael Alex Kiria, Bi. Sophia Hussein Kizenga, Bw. John Leslie Limu; na Bi. Haleleki Juma Salehe.

shughuli zake, ikiwemo kuwezesha watumishi wa Tume kufanya ziara shuleni kwa lengo la kusikiliza na kutatua changamoto za walimu kwa wakati.

Bi. Sophia aliishukuru Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu kwa kuendelea kutoa mafunzo ya usimamizi wa mashauri ya kinidhamu na rufaa za walimu, ambayo yameongeza uwezo na uelewa wa watumishi katika kushughulikia mashauri kwa kuzingatia sheria na taratibu, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walitegemea zaidi uzoefu binafsi.

Alisema pia kuanzishwa kwa Mfumo wa Taarifa za Utumishi wa Walimu (TSCMIS) kumerahisisha usajili wa walimu wapya na utoaji wa namba za usajili mara baada ya kukamilisha taratibu za ajira, tofauti na zamani ambapo walimu walilazimika kusubiri kwa muda mrefu kupata namba hizo.

Kwa kipindi cha mwaka 2024 hadi 2026, alisema walimu 94 wamesajiliwa kupitia mfumo huo, kati yao 30 ni walimu wa shule za msingi na 64 ni walimu wa shule za sekondari.

Akizungumzia mafanikio mengine, Bi. Sophia alisema TSC imeendelea kuboreshwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa vya ofisi, ikiwemo kompyuta mpakato (laptop), printa na pikipiki kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu. Aliongeza kuwa baadhi ya wilaya zimepatwa magari ya kazi, hatua inayoongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume na kuboresha huduma kwa walimu.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kisarawe, Bi. Sophia Hussein Kizenga, akiwa ofisini kwake wakati wa mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali.

BALOZI MUTATEMBWA AIPONGEZA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KWA UTOAJI WA HUDUMA BORA



Balozzi wa Tanzania nchini Japan, Mhe. Anderson Mutatembwa (kushoto), akisikiliza maelezo kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) alipotembelea banda la Tume lililopo ndani ya Banda la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam, tarehe 1 Julai 2026.

Na Mwandishi wetu – Dar es Salaam

Balozzi wa Tanzania nchini Japan, Mhe. Anderson Mutatembwa, tarehe 1 Julai 2026 ametembelea banda la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba) yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Akiwa katika banda hilo, Mhe. Mutatembwa alipata fursa ya kutembelea Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), ambapo alijionea huduma mbalimbali zinazotolewa na Tume kwa walimu na wadau wa sekta ya elimu.

Mhe. Mutatembwa ameipongeza TSC kwa kazi nzuri inayofanya katika kushughulikia masuala ya walimu kwa wakati, jambo ambalo amesema limechangia kuimarisha utulivu na kuongeza ari ya walimu katika kutekeleza majukumu yao ya kuwahudumia wanafunzi na Taifa kwa ujumla.

Amesema juhudi zinazofanywa na Tume katika kusimamia na kutatua changamoto za walimu zina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji kazi wa sekta ya elimu, hivyo ni muhimu kuendelea kuziimarisha.

Aidha, amewahimiza watumishi

wa Tume kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa bidii, weledi na ubunifu ili kuhakikisha walimu wanaendelea kupata huduma bora, zenye ufanisi na zinazokidhi matarajio yao.



Balozzi wa Tanzania nchini Japan, Mhe. Anderson Mutatembwa (kushoto), akizungumza na mtoa huduma katika banda la TSC alipotembelea Banda la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam, tarehe 1 Julai 2026.

BALOZI MUTATEMBWA AIPONGEZA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KWA UTOAJI WA HUDUMA BORA



Balozi wa Tanzania nchini Japan, Mhe. Anderson Mutatembwa (kushoto), akizungumza na mtoa huduma katika banda la TSC alipotembelea Banda la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Vizwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam, tarehe 1 Julai 2026.



Balozi wa Tanzania nchini Japan, Mhe. Anderson Mutatembwa, akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) lililopo ndani ya Banda la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea katika Vizwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam, tarehe 1 Julai 2026.



Picha za matukio mbalimbali katika maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika tarehe 16 hadi 23 Juni, 2026 jijini Dodoma.



Picha za matukio mbalimbali katika maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika tarehe 16 hadi 23 Juni, 2026 jijini Dodoma.



Picha za matukio mbalimbali katika maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika tarehe 16 hadi 23 Juni, 2026 jijini Dodoma.

MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA MKURANGA YAMEONGEZA UELEWA WA SHERIA NA TARATIBU ZA UTUMISHI

Na Mwandishi Wetu, Mkuranga

Mafunzo elekezi yanayotolewa kwa walimu wa ajira mpya katika Wilaya ya Mkuranga yamechangia kuwaongezea uelewa kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma, hatua iliyowasaidia kutambua haki, wajibu na maadili ya kazi wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkuranga, Bi. Christina F. Ngalawa, wakati wa mahojiano na Afisa wa

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC kuhusu mafanikio ya miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Tume hiyo.

Bi. Ngalawa alisema mafunzo hayo yamekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha nidhamu kwa walimu, hali iliyosaidia kupunguza idadi ya mashauri ya nidhamu kutoka wastani wa mashauri 133 kwa mwaka katika kipindi cha 2016–2020 hadi kufikia wastani wa mashauri 34 kwa mwaka katika kipindi cha 2021–2025.

Aidha, alisema TSC imeendelea kuwajengea uwezo viongozi wa elimu kwa kutoa mafunzo ya ufafanuzi wa Kanuni na Maadili ya Utumishi kwa wakuu wa shule za msingi 127, hatua iliyowawezesha kutekeleza kwa ufanisi majukumu yao kama Mamlaka za Nidhamu katika shule wanazosimamia.

Akizungumzia mafanikio mengine ya Tume katika kipindi cha miaka kumi, Bi. Ngalawa alisema walimu 535 waliokuwa wamejiendeleza kielimu walibadilishiwa miundo ya utumishi katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Aliongeza kuwa kuanzia mwaka 2021 hadi 2025 jumla ya walimu 2,713 walipandishwa vyeo, huku walimu 257 wakipandishwa vyeo kwa njia ya mserereko katika miaka ya fedha 2023/2024 na 2024/2025.

Bi. Ngalawa pia aliishukuru Serikali kwa kuwezesha uanzishwaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS), ambao umeimarisha utoaji wa huduma kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za walimu kwa haraka na kwa wakati. Alisema mfumo huo unahifadhi taarifa muhimu zikiwemo usajili wa walimu, mikataba ya ajira, barua za ajira na namba za usajili wa TSC.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiparang'anda ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Wilaya ya TSC, Mwl. Fatma J. Karama, alisema muundo wa kamati unaowajumuisha wawakilishi wa walimu kutoka shule za msingi na sekondari umeongeza uwazi katika utoaji wa maamuzi na kurahisisha kuwafikia walimu wote kwa wakati.

Naye Mwalimu wa Shule ya Msingi Ngongoti, Mwl. Edina E. Kanoni,



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiparang'anda na Mjumbe wa Kamati ya Wilaya ya TSC, Mwl. Fatma J. Karama, akizungumza wakati wa mahojiano kuhusu mafanikio ya miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu.

aliipongeza TSC kwa kuendelea kufanya ziara za mara kwa mara shuleni kwa lengo la kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili walimu na kuzitafutia ufumbuzi kwa wakati, jambo ambalo limeongeza imani ya walimu kwa Tume na kuboresha utoaji wa huduma.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Ngongoti, Mwl. Edina E. Kanoni, akizungumza wakati wa mahojiano maalumu kuhusu mafanikio ya miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkuranga, Bi. Christina F. Ngalawa, akiwa ofisini kwake akitekeleza majukumu ya kila siku.

**MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA MKURANGA
YAMEONGEZA UELEWA WA SHERIA NA TARATIBU ZA UTUMISHI**

Picha ya pamoja ya watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga na baadhi ya walimu waliotembelea ofisi za Tume zilizopo katika jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga. Kutoka kulia ni Mwl. Fatma J. Karama wa Shule ya Sekondari Kiparang'anda, Mwl. Edina E. Kanoni wa Shule ya Msingi Ngongoti, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mkuranga Bi. Christina F. Ngalawa, na kushoto ni Bw. Stephen Christian Lucas.

TSC MOMBA YAPONGEZWA KWA KUTOA ELIMU NA KUSOGEZA HUDUMA KARIBU NA WALIMU

Na Mwandishi Wetu, Momba

Baadhi ya walimu Wilaya ya Momba mkoani Songwe wameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuendesha ziara za utoaji wa elimu na kusogeza huduma karibu na walimu, hatua iliyowezesha kusikiliza na kutatua kero pamoja na changamoto zinazowakabili katika utumishi wao.

Akizungumza, Mwalimu wa Shule ya Msingi Katete iliyopo Kata ya Mpemba, Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Mwl. Ndinhesya Angetile alisema ziara hizo zimewasaidia walimu kupata uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu, jambo lililochangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Elimu tunayoipata kutoka Tume imetusaidia kufahamu haki, wajibu na taratibu za kiutumishi, hivyo kuturahisishia kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo," alisema.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Katete, Mwl. Ndinhesya Angetile, akizungumzia mafanikio ya Tume ya Utumishi wa Walimu katika kipindi cha miaka kumi tangu kuanzishwa kwake.

Naye Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mpemba, Mwl. Baraka Mnyemba alisema kuwa katika kipindi cha miaka kumi tangu kuanzishwa



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mpemba, Mwl. Baraka Mnyemba, akielezea maboresho yaliyofikiwa katika utatuzi wa changamoto za walimu tangu kuanzishwa kwa TSC ikilinganishwa na kipindi cha awali.

kwa Tume ya Utumishi wa Walimu, kumekuwa na maboresho makubwa katika utatuzi wa changamoto za walimu zilizokuwa zikidumu kwa muda mrefu.

Alisema changamoto zinazohusu kupandishwa vyeo, kubadilishiwa muundo wa kada, pamoja na kulipwa stahiki zinazotokana na mabadiliko hayo sasa zinapatiwa ufumbuzi kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa kwa Tume.

"Kwa sasa changamoto nyingi zilizokuwa zikiwasumbua walimu zimepungua kwa kiwango kikubwa. Hali hii imeongeza ari na morali ya walimu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Momba, Mwl. Ferdinand Hakanigwa William alisema kuwa kwa kipindi cha miaka kumi ya utekelezaji wa majukumu yake, Tume imefanikiwa kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa Tume, walimu walikabiliwa na changamoto mbalimbali, hususan katika masuala ya upandishaji vyeo, mabadiliko ya muundo wa kada na upatikanaji wa stahiki, lakini hali hiyo imeimarika kwa kiasi kikubwa



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Momba, Mwl. Ferdinand Hakanigwa William, akielezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Tume mwaka 2016.

kutokana na maboresho yaliyofanywa na Tume.

Aidha, alisema Serikali imeendelea kuiwezesha Tume kuimarisha ofisi za wilaya ili ziweze kuwafikia walimu kwa karibu zaidi, hatua iliyopunguza gharama na muda waliokuwa wakitumia kufuatilia huduma mbalimbali za kiutumishi.

Mwl. Hakanigwa aliongeza kuwa matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yameongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu, kwa kuwa yamepunguza ulazima wa kusafiri umbali mrefu kufuatilia masuala ya kiutumishi.

Vilevile, alisema Serikali imeiwezesha Tume kuendesha mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya, yanayolenga kuwajengea uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kupunguza mashauri ya nidhamu, jambo ambalo halikuwa likifanyika kabla ya kuanzishwa kwa Tume.

MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU AJIRA MPYA YAIMARISHA UTENDAJI WA KAZI WILAYANI BAGAMOYO



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bagamoyo, Bw. Azizi Metta, akiwa ofisini kwake akitekeleza majukumu ya kazi.

Na Mwandishi Wetu, Bagamoyo

Mafunzo elekezi yanayotolewa kwa walimu wa ajira mpya katika Wilaya ya Bagamoyo yamechangia kuwaongezea uelewa kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi, hatua iliyosaidia kuimarisha utendaji wao wa kazi na utoaji wa huduma katika sekta ya elimu.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bagamoyo, Bw. Azizi Metta, alipokuwa akielezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha

miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Tume.

Bw. Metta alisema kupitia mafunzo hayo, walimu wa ajira mpya hupata fursa ya kukutana na taasisi mbalimbali zinazotoa huduma muhimu kwa watumishi wa umma, zikiwemo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Shirika la Bima la Taifa (NIC) pamoja na taasisi mbalimbali za kifedha. Alisema taasisi hizo huwapatia walimu elimu kuhusu huduma wanazostahili na namna bora ya kuzifikia.

Aidha, alisema mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuanzishwa kwa Mfumo wa TSCMIS, ambao umeongeza ufanisi katika utoaji wa

huduma kwa walimu. Kupitia mfumo huo, walimu wamekuwa wakipatiwa kwa wakati namba za usajili, barua za ajira, uthibitisho kazini pamoja na mikataba ya ajira.

Aliongeza kuwa mfumo huo umeboresha pia usimamizi wa mashauri ya kinidhamu kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa haraka na kurahisisha utoaji wa maamuzi kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo mashauri hayo yalichukua muda mrefu kushughulikiwa.

Bw. Metta pia aliipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuendelea kuzipatia ofisi za TSC katika wilaya rasilimali fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali, ikiwemo vikao vya kisheria na uchunguzi wa mashauri ya kinidhamu. Alisema hatua hiyo imeongeza ufanisi katika utoaji wa haki kwa walimu kwa kushughulikia mashauri yao kwa wakati.

Vilevile, alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha maslahi ya walimu kupitia upandishaji wa vyeo, mabadiliko ya kada kwa walimu waliojiendeleza kielimu pamoja na ulipaji wa stahiki mbalimbali kwa wakati.

Alisema hatua hizo zimepunguza changamoto zilizokuwa zikiwakabili walimu kwa muda mrefu na kuongeza ari ya kazi, hivyo kuchangia kuboresha utoaji wa huduma za elimu nchini.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bagamoyo, Bw. Azizi Metta (kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa ajira mpya baada ya kuhitimisha mafunzo elekezi.

TSC RUFJI YAJIVUNIA MAFANIKIO YA MFUMO WA TSCMIS KATIKA KUBORESHA HUDUMA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu, Rufiji

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rufiji imeeleza kuwa matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) yameleta mapinduzi makubwa katika utoaji wa huduma kwa walimu kwa kurahisisha usimamizi wa taarifa na kuimarisha utoaji wa maamuzi kwa wakati.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Rufiji, Bi. Gloria Liwongwe, wakati wa mahojiano na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake.

Bi. Liwongwe alisema mfumo wa TSCMIS umeunganishwa na mifumo mingine ya Serikali, hatua inayowezesha kubadilishana taarifa muhimu za walimu kwa haraka na kwa usahihi.

Alisema matumizi ya mfumo huo yameongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa taarifa za walimu, utoaji wa taarifa kwa mamlaka husika, pamoja na kurahisisha upatikanaji wa barua za ajira na namba za utambulisho wa walimu (TSC Number), tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo walimu walilazimika kusubiri kwa muda mrefu kupata huduma hizo kutoka Makao Makuu.

Aidha, alisema mfumo huo umeboresha usimamizi wa mashauri ya nidhamu kwa kuwa unaainisha makosa, adhabu zinazostahili na hatua za kuchukua kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizopo. Alibainisha kuwa hali hiyo imeongeza uwazi, kuharakisha utoaji wa maamuzi na kuboresha uendeshaji wa mashauri ya nidhamu.

"Kupitia mfumo huu, mashauri yanashughulikiwa kwa haraka zaidi na kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa, jambo ambalo limeongeza ufanisi katika utendaji wa Tume," alisema Bi. Liwongwe.

Akizungumzia mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ya TSC, Bi. Liwongwe alisema Serikali imeendelea kuwifanyia majukumu ya kazi kwa haraka na kuboresha huduma kwa walimu.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Rufiji, Bi. Gloria Liwongwe, akiwa ofisini akiendelea na majukumu yake ya kila siku.

Tume kwa kuvipatia vyombo vya usafiri ikiwemo pikipiki na magari katika baadhi ya wilaya, hatua iliyoongeza uwezo wa kuwafikia walimu waliopo katika maeneo mbalimbali.

Alisema uwepo wa vyombo hivyo umewezesha watumishi wa TSC kufanya ziara za mara kwa mara shuleni kwa ajili ya kusikiliza na kutatua changamoto za walimu, kutoa elimu kuhusu masuala ya kiutumishi na kushughulikia hoja mbalimbali kwa wakati.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Sekondari Utete, Mwl. Mussa Nassor Kinina, ameipongeza TSC kwa kuanzisha mafunzo elekezi kwa walimu wapya, akisema yamekuwa na mchango mkubwa katika kuwajengea uelewa kuhusu haki, wajibu na maadili ya utumishi wa umma.

Alisema mafunzo hayo yanawawezesha walimu kuanza kazi wakiwa na uelewa mzuri wa majukumu yao, tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo walimu wengi walikosa mwongozo rasmi walipoajiriwa.

Mwl. Kinina pia alipongeza maboresho yaliyofanyika katika kushughulikia upandishaji wa vyeo na utekelezaji wa mishahara mipya



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Utete, Mwl. Mussa Nassor Kinina, akizungumza wakati wa mahojiano maalum na Afisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu.

kwa wakati, akisema hatua hiyo imeondoa changamoto ya walimu kusubiri kwa muda mrefu kupata stahiki zao.

Naye Mwalimu wa Shule ya Msingi Utete, Mwl. Genoveva Evarist Basheka, alisema TSC imeleta maboresho makubwa katika mchakato wa kubadilisha muundo wa utumishi kwa walimu wanaojiendeleza kielimu.

Alisema kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025, walimu wanaokamilisha masomo yao wanabadilishwa muundo wa utumishi kwa wakati bila kuathiri tarehe zao za kupandishwa cheo, tofauti na ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa kwa TSC.

Aidha, alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuimarisha sekta ya elimu kupitia maboresho mbalimbali yanayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema maboresho hayo, pamoja na kuanzishwa kwa muundo mpya wa watumishi wa TSC, yameongeza ufanisi wa Tume katika kutoa huduma kwa walimu na ni sehemu ya mafanikio makubwa yanayoadhimishwa katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu